# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME

## NGOME SACCOS LTD

## (DSR 991)

# SERA YA UWEKEZAJI

TOLEO LA I : 2020

# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NGOME

## NGOME SACCOS LTD

## (DSR 991)

# SERA YA UWEKEZAJI

TOLEO LA I : 2020

# YALIYOMO


UKURASA

*DIBAJI* .......... 2

SEHEMU YA KWANZA .......... 4

1.0 UTANGULIZI .......... 4

1.1 Historia fupi ya Chama .......... 4

1.2 Mawanda ya Sera .......... 4

1.3 Madhumuni ya Sera ya uwekezaji .......... 5

SEHEMU YA PILI .......... 5

2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA .......... 5

2.1 Maeneo ambayo chama kinaweza kuwekeza .......... 5

2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya kufanya uwekezaji .......... 6

2.3 Muda wa kuiva wa uwekezaji .......... 7

SEHEMU TATU .......... 7

3.0 NAMNA YA KUPUNGUZA VIHATARISHI .......... 7

SEHEMU YA NNE .......... 8

4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU .......... 8

4.1 Mamlaka ya Uwekezaji .......... 8

4.2 Kamati ya Uwekezaji .......... 8

4.2.1 Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji .......... 8

SEHEMU YA TANO .......... 9

5.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI .......... 9

SEHEMU YA SITA .......... 10

HITIMISHO .......... **Error! Bookmark not defined.**

# DIBAJI

Sera hii ya uwekezaji ya NGOME SACCOS LTD imeandaliwa na Bodi ya chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni za Huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019. Sera hii inatoa mwongozo sahihi wa uwekezaji wa chama kuwekeza katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia kifungu cha 74 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya (49 - 50) ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2019.

Bodi na menejimenti wakati wote itawekeza kwa maslahi mapana ya wanachama na Chama kwa kuzingatia sera hii.

Sera hii imejumuisha Sehemu Sita, **Sehemu ya kwanza** ni utangulizi, s**ehemu ya pili ni** umuhimu wa uwekezaji, **sehemu ya tatu** ni maeneo ya uwekezaji (Investment destinations), **sehemu ya nne** ni Kuiva kwa uwekezaji na hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa uwekezaji (Investment maturity and Risks) , **Sehemu ya tano** ni Utoaji wa taarifa za uwekezaji kwa Bodi ya chama na **Sehemu ya Sita** ni Hitimisho.

## SEHEMU YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Historia ya Chama

NGOME SACCOS Ltd yenye nambari ya usajiri DSR 991 Ilisajiriwa tarehe 30, April 2007 chini ya Sheria ya Ushirika Na 20 ya mwaka 2003 kama ilivyorejewa na sheria ya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 na baadae Sheria mpya ya huduma ndogo za fedha ya mwaka 2018 kama ushirika wa fedha wenye ukomo wa dhima ili kutoa huduma za akiba na mikopo kwa Wanachama wake. Wanachama wa NGOME SACCOS Ltd ni Maafisa ,Maaskari , Wastaafu pamoja na Watumishi wa Umma wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wale waliohamia wizara nyingine wakiwa wanachama Hai wa Ngome SACCOS.

## 1.2 Mawanda ya Sera

Sera hii inatoa mwongozo wa kisheria na uwazi katika uwekezaji wa aina mbalimbali utakaofanywa na chama kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na kanuni zake, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya mwaka 2018 na Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (SACCOS) ya mwaka 2019.

Sera hii itatumika wakati wote kama mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kufanya maamuzi ya uwekezaji (Investment decisions) kwa maslahi mapana ya wanachama na chama.

## 1.3 Madhumuni ya Sera ya uwekezaji

i. Kuainisha majukumu ya pande zote zitakazohusika katika Uwekezaji
ii. Kuweka utaratibu utakaozingatiwa katika mchakato wa maamuzi ya uwekezaji
iii. Kuweka uelewa wa pamoja kwa wahusika wote juu ya malengo ya uwekezaji
iv. Kutoa mwongozo na ukomo wa uwekezaji utakaofanywa na Chama
v. Kuweka mwongozo wa kufanya tathimini ya uwekezaji
vi. Kupima kama uwekezaji uliofanyika unasimamiwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MAENEO AMBAYO CHAMA KINATAKIWA KUWEKEZA

Shughuli kuu ya chama ni kupokea akiba za wanachama na kutoa mikopo kwa wanachama wake. Hivyo kipaumbele cha uwekezaji wa fedha za chama utakuwa ni kutoa mikopo kwa wanachama wake.

## 2.1 Maeneo ambayo chama kinaweza kuwekeza

Chama kitawekeza kwenye maeneo mengine endapo chama kitakuwa na ukwasi toshelevu, hivyo chama kinaweza kuwekeza katika maeneo yafuatayo:.

i. Kuwekeza fedha kwenye benki kama Amana za muda maalumu (FDR).
ii. Kuwekeza kwenye taasisi nyingine za fedha kama vile ununuzi wa vipande UTT au hisa katika kampuni zinazofanya vizuri katika soko la Hisa (DSE).
iii. Kuwekeza katika dhamana za Serikali (Government Securities).
iv. Kuwekeza kwenye SACCOS na Vyama vya Ushirika vya upili (second tier or secondary cooperative societies)
v. Kuwekeza katika mali zisizozalisha (Non-Earning assets) kama vifaa, majengo na ardhi ambapo;

a) Chama kitawekeza katika mali zisizozalisha (non-earning assets / property / Equipment) kwa kiwango kisichozidi asilimia 10 % ya mali zote za chama.
b) Uwekezaji katika ardhi na majengo hautazidi asilimia 5% ya mali zote za chama

vi. Chama kinaweza kuingia ubia katika uwekezaji kwa idhini ya MRAJIS baada ya kutengeneza mkataba unaonesha haki na wajibu wa kila mbia. Endapo Viongozi ama Watendaji ni wabia katika uwekezaji wa Chama, sehemu ya umiliki wao kwa ujumla hautatakiwa kuzidi 10% kama inavyoelekezwa kwenye kanuni ya vyama vya akiba na mikopo kanuni 88(2).

Aidha, chama kinaweza kuwekeza katika mradi wowote ambao utaruhusiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

## 2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya kufanya uwekezaji

Kabla ya kufanya maamuzi ya kuwekeza, chama kitafanya upembuzi wa kina kikizingatia mahitaji ya wanachama na hali halisi ya ukwasi na vipindi vya mahitaji makubwa ya mikopo kwa wanachama. Chama kitakapohitaji kuwekeza, kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Kufanya tathimini ya kina juu ya mahitaji na uwezo wa kifedha wa chama.
ii. Muda wa kuiva kwa uwekezaji husika (Investment Maturity).
iii. Mapato tarajiwa toka kwenye uwekezaji husika (Return on investment) yasiwe chini ya riba inayotozwa katika utoaji wa mikopo.
iv. Vihatarishi kwenye uwekezaji (Investment risks).
v. Hali ya utendaji wa chama (Performance trend analysis).
vi. Sera za uwekezaji za Sekta husika.
vii. Historia ya taasisi itakayowekezwa.
viii. Gharama za uwekezaji.
ix. Chama hakitatakiwa kutumia uwekezaji kama dhamana ya mkopo nje bila idhini ya MRAJIS .
x. Na mambo mengine kulingana na mazingira husika.

## 2.3 Muda wa kuiva kwa uwekezaji

Chama kitawekeza katika maeneo ambayo, muda wa uwekezaji utazingatia miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na mamlaka nyingine juu ya ukomo wa muda wa uwekezaji husika.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 NAMNA YA KUPUNGUZA VIHATARISHI

Chama kinatakiwa kufanya uwekezaji kwenye maeneo tofauti tofauti (Portfolio diversification) ili kupunguza hatari ya kupata hasara kubwa. Hivyo, pamoja na mambo mengine, uwekezaji utatakiwa kuzingatia mambo matatu ambayo ni usalama, ukwasi na faida tarajiwa. Usalama wa uwekezaji utakuwa ndio lengo kuu la mpango wa uwekezaji.

Ili kupunguza hatari katika uwekezaji, Chama kitatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Chama hakitaweka fedha katika benki moja au taasisi moja ya kifedha kwa kiwango kinachozidi asilimia 25% ya mtaji tete wa chama kwa ajili ya kufanya mtawanyo wa vihatarishi (diversification of risks or risks spread), isipokuwa kama itaidhinishwa na mamlaka husika ya usimamizi kama Tume ya Ushirika.

ii. Chama kitatakiwa kufanya uwekezaji kwenye maeneo salama yaliyotajwa kwenye Sera hii katika sehemu ya pili.

iii. Chama kinatakiwa kufanya uwekezaji kwenye dhamana za muda mfupi na mrefu, masoko ya fedha na kudhibiti muda wa uwekezaji.

iv. Endapo Chama kitapata hasara katika uwekezaji, uchunguzi maalum utafanyika na ikigundulika kuwa taratibu zote zilifuatwa na kulikuwa na nia njema isipokuwa hasara imetokana na hali nje ya uwezo wa Chama; kinga iliyopo katika kifungu cha 135 cha Sheria ya Ushirika na 6 ya 2013 itatumika.

Endapo itathibitika hasara ya uwekezaji imesababishwa na Bodi kwa uzembe ama nia ovu yoyote; kifungu cha 74 (3) na kifungu cha 126 vya Sheria ya Ushirika na 6 ya mwaka 2013 vinatoa adhabu kwa kukisababishia Chama hasara.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAMLAKA YA KUFANYA UWEKEZAJI NA MGAWANYO WA MAJUKUMU

### 4.1 Mamlaka ya Uwekezaji

#### 4.1.1 Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama

Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama utakuwa na mamlaka ya kupitisha aina yoyote ya uwekezaji unaotakiwa kufanywa na Chama kama ilivyopendekezwa na Bodi kwa kadri itakavyoonekana inafaa. Aidha, baada ya Mkutano Mkuu kupitisha, Chama kitatakiwa kupeleka maombi ya kuidhinishiwa uwekezaji huo kwa MRAJIS.

### 4.2 Kamati ya Uwekezaji.

Kamati ya Uwekezaji itaundwa na bodi, kamati itakuwa na watu watano, kati yao wawili (2) watakuwa watendaji, wawili(2) watakuwa ni wajumbe wa Bodi iliyopo madarakani na mmoja (1) kiongozi wa Chama aliyemaliza muda wake akitumikia chama kwa Uaminifu na Uadilifu, pia anatakiwa kuwa na elimu ya fedha na Uchumi. Kamati hii itaripoti kwa Bodi.

### 4.2.1 Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji

Kamati itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kufanya tathmini ya vihatarishi katika uwekezaji na mipaka ya uwekezaji na kutoa taarifa kwa Bodi.

ii. Kupendekeza kwa Bodi fursa zozote za uwekezaji kulingana na mwenendo wa uchumi uliopo .

iii. Kuishauri Bodi juu ya Uwekezaji wenye tija.

iv. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya uwekezaji na kuiwasilisha kwenye Vikao vya Bodi.

v. Kuishauri Bodi juu ya mabadiliko ya sera hii.

N.B Endapo Kamati hii itasababishia chama hasara itawajibika kwa mujibu wa sheria Na 6 ya Ushirika ya mwaka 2013.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI

Menejimenti ya chama itatakiwa kutoa taarifa ya uwekezaji kwa Bodi ya chama angalau kila mwezi au isizidi robo mwaka. Taarifa hiyo itaainisha pamoja na mambo mengine, mambo makuu yafuatayo;

i. Aina zote za uwekezaji uliofanywa na chama.
ii. Riba halisi ya kila uwekezaji mpaka siku taarifa hiyo inapotolewa.
iii. Tarehe ya kuiva kwa kila uwekezaji na taarifa nyingine zinazohusiana na uwekezaji.
iv. Shughuli za uwekezaji za kila mwezi kama vile kununua na kuuza, na riba iliyorejeshwa.
v. Malinganisho ya kwenye vitabu (book value) na malinganisho ya soko kwa wakati husika (current market value).
vi. Na taarifa nyingine muhimu kama zipo.

## HITIMISHO

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya Ngome SACCOS na Kamati ya Usimamizi iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua yenye kumbukumbu Na. MA.82/309/20/14 ya tarehe 05 AGOSTI, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

Mwenyekiti

Katibu

NGOME SAVING AND CREDIT CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED
NGOME SACCOS LTD
REG. DSR 991
P. O. Box 35923
DAR ES SALAAM

TANZANIA
Approved this 01st
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies